


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA ELIMU NA UTAMADUNI

Aenezi ya Simu: "ELIMU" DAR ES SALAAM  
SIMU: 110146-52  
Teleo: 41742 Elimu Tz  
Fax: 255-51-113271 Elimu Tz  
Unapojibu tufadhali taja:



SANIKU LA POSTA 9121  
DAR ES SALAAM

Kumbu Namba: ED/OK/C.2/4/59

Tarehe: 6/10/1998


Makalibu Tawala Mikoa,  
Makalibu Tawala Wilaya,  
Wakaguzi Wakuu wa Kanda,  
Wakuu wa Mafunzo ya Ualimu,  
Wakuu wa Shule za Sekondari

WARAKA WA ELIMU NA: 5 WA MWAKA 1998  
SOMO LA DINI

Wizara ya Elimu na Utamaduni inapenda kutoa ufafanuzi kuhusu Somo la Dini kufuatia Waraka wa Elimu Namba 1 na Namba 2 wa mwaka 1993 Kumb. Na. ED/OKE/S.4/24 na ED/OKE/S.4/25 zote za tarehe 10/5/1993 kuhusu Muundo mpya wa masomo.

- a. Mafundisho ya Dini katika Shule za Msingi na Sekondari ni ya lazima.
- b. Somo la Dini linapaswa kupangiwa vipindi viwili kwa wiki katika shule za Msingi Darasa la 1-7 na Shule za Sekondari, kidato cha 1-6.
- c. Mafundisho ya Dini yatafundishwa na walimu wa dini wa madhehebu yote yanayotambulika nchini.
- d. Wakuu wa Shule na Vyuo watatakiwa kushirikiana na madhehebu ya dini yaliyo karibu na shule ili kupata walimu wanaofundisha somo hilo. Pia walimu wa shule wenye sifa na kupenda kufundisha somo hili wahamasishwe na kukubaliwa.
- e. Licha ya mafundisho ya Dini kuwa ya lazima, Dini inaweza kusomwa kama somo la ziada (additional and Examinable options) ambalo mwanafunzi atatahiniwa kama somo lingine katika Mitihani ya Taifa. Aidha mafundisho ya Dini yafanyiwe tathmini na alama zake ziandikwe kwenye ripoti ya kila muhula kwa kila mwanafunzi. Mitihani itatungwa na kusahihishwa na wimu wanaofundisha somo hilo lakini litolewe na kusimamiwa na walimu wa shule.

Wakuu wa Shule na Vyo wanatakiwa kuyapa uzito na umuhimu mafunzo ya Dini kwa wanafunzi, kwa vile yanachangia kujenga na kuwapa maadili mema vijana wa shule.



A.S. Ndeki  
KAMISHNA WA ELIMU